JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA**

**Kumb. Na.** WPF/0062/2 **Tarehe:** 09/01/2026

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi tano (05) katika Manispaa hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

## 1.0. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA II – NAFASI 5

### 1.1. MAJUKUMU NA KAZI

i. Kuorodhesha barua zinazoingia masijala kwenye Regista (Incoming Correspondence Register)
ii. Kuorodhesha barua zinazo toka nje ya Taasisi (Outgoing Correspondence Register)
iii. Kusambaza majalada kwa watendaji (Action Officers)
iv. Kupokea majalada yanayo rudi masijala kutoka kwa watendaji
v. Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (Racks/Filling cabinets) au Mahali pengine yanapo hifadhiwa.
vi. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani na nje ya Taasisi (File tracking)
vii. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (classification and boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
viii. Kuweka Kumbukumbu (barua,nyaraka n.k) katika mafaili.
ix. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa na msimamizi wake wa kazi.

**1.1.1. SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa mwenye Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au cha Sita (VI) aliye hitimu mafunzo ya stashahada/Diploma (NTA Level 6) katika fani ya utunzaji wa kumbukumbu kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, wenye ujuzi wa kutumia kompyuta.

**1.1.2. NGAZI YA MSHAHARA**

**TGS C**

**MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wawe Watanzania wenye umri kuanzia Miaka **18** na usiozidi miaka **45** .

**ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuanisha kwenye mfumo wa kuombea ajira aina ya Ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.**

iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza Curriculum Vitae (CV) yenye Anuani inayotumika, namba ya simu zinazopatikana na Anuani ya barua pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika. “Provisional “Testimonials” Statement of results” na hati za matokeo za kidato cha Nne na Sita (Form IV na Form VI results slip **HAVITAKUBALIWA**

iv. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.

v. Waombaji walio staafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

vi. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingia katika Kada hiyo wapitishe barua kwa waajiri wao na waajiri wao wajiridhishe sfa zao ipasavyo.

vii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma, wasiombe bali wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika **Waraka Na.CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**

viii. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma vilivyo thibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne,Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango cha vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika, kama vile.

ix. Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificate, - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV Na Vi, - Computer Certificate – Vyeti vya kitaaluma (Professional Certificate from Respective Boards)

x. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimethibitishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA au NACTVET).**

xi. Uwasilishaji wa Taarifa na sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria,

xii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza

xiii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **22 Januari ,2026**

xiv. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu,aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:

**Mkurugenzi wa Manispaa,**
**Manispaa ya Tabora,**
**4 Barabara ya Kiwanja cha Ndege,**
**S.L.P 174,**
**45182 TABORA**

xv. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa kielektoniki wa ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatavyo**;** https://portal.ajira.go.tz Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa “Recruitment Portal”

xvi. Maombi yatakayo wasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

**Limetolewa na:-**

**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**MANISPAA YA TABORA**